# Barua kuhusu Haki za watu waliozuiliwa chini ya Sheria ya Ugaidi ya 2000

Kipeperushi hiki kinakupa taarifa muhimu kuhusu haki zako kulingana na sheria nchini Uskoti ukiwa umezuiliwa katika kituo cha polisi. Hati hii inakueleza kuhusu haki zako kuu unapowekwa kizuizini. Sio ushauri wa kisheria na haikuelezi kuhusu haki zako zote. Unapaswa kutafuta ushauri wa kisheria kivyako.

Tafadhali soma taarifa hizi haraka iwezekanavyo. Zitakusaidia kufanya maamuzi ukiwa katika kituo cha polisi. Tafadhali waambie polisi wakueleze chochote usichokielewa katika kipeperushi hiki, ikiwa unataka nakala iliyo rahisi kusoma au tafsiri.

Kumbuka haki zako:

- Una haki ya kujua kwa nini umezuiliwa na polisi.
- Una haki ya wakili kujulishwa kuwa uko katika kituo cha polisi. Hutalipishwa kwa hili.
- Una haki ya mtu mwingine anayejali maslahi yako kujulishwa kuwa uko polisi. Kwa mfano, huyu anaweza kuwa mwanafamilia, mlezi au rafiki.
- Una haki ya kukaa kimya. Sio lazima ujibu maswali unayoulizwa na polisi. LAKINI unahitajika kusema jina lako, anwani, tarehe ya kuzaliwa, mahali ulipozaliwa na utaifa wako.
- Una haki ya kuzungumza na wakili faraghani kabla ya polisi kukuhoji. Unaweza pia kuzungumza na wakili wakati wowote polisi wanapokuuliza maswali.
- Ikiwa una umri wa chini ya miaka 16, au hujafikisha miaka 18 na uko chini ya uangalizi, pia una haki ya kutembelewa na mzazi au mlezi wako katika kituo cha polisi.
- Una haki ya kupata usaidizi wa haraka wa kimatibabu.
- Una haki ya kulalamika kuhusu jinsi umetendewa na polisi.

## Haki zako

Tafadhali kumbuka: Wakati mwingine ikihitajika, polisi wana haki ya kuchelewesha kutekeleza au kukuzuia kupata baadhi ya haki hizi. Kwa mfano, ikiwa polisi wanaamini kuwa wanahitaji kukuhoji ili kuzuia mtu mwingine kuumizwa. Hii haijumuishi haki yako ya kukaa kimya.

### 1. Taarifa kwa watu wanaozuiliwa na polisi

- #### Kujua sababu ya kukamatwa na kuwekwa kizuizini

Polisi wanapaswa kukueleza sababu za kukamatwa na kushukiwa kuhusika katika kufanya, kupanga au kuchochea ugaidi.

Kituoni, polisi lazima wakujulishe ni kwa nini wanaamini unahitaji kuzuiliwa.
Kabla ya kuulizwa maswali yoyote kuhusu tuhuma yako ya kuhusika na ugaidi, polisi lazima wakupe wewe au wakili wako taarifa za kutosha kuhusu kile wanachoamini umefanya ili uweze kujitetea lakini bila kuathiri uchunguzi wao.

- #### Haki ya Kukaa kimya

Unaweza kukaa kimpya unapoulizwa maswali na polisi kuhusu kile wanachoamini umefanya.

Chochote utakachosema kitaandikwa au kurekodiwa na kinaweza kutumika kama ushahidi katika mashtaka, kesi yako ikipelekwa mahakamani.

Ni lazima uwaambie polisi jina na anwani, tarehe ya kuzaliwa, mahali pa kuzaliwa na utaifa wako wanapokuuliza maelezo haya.

- #### Kumfahamisha Wakili kwamba uko katika kituo cha polisi

Unaweza kuwaomba polisi wamfahamishe wakili kwamba uko katika kituo cha polisi. Huyu anaweza kuwa wakili wako mwenyewe au, ikiwa huna wakili, wakili wa zamu hiyo. Polisi watapanga wakili apigiwe haraka iwezekanavyo. Hutalipishwa chochote kwa hili.

Kumfahamisha mtu mwingine anayejali maslahi yako kwamba uko kwenye kituo cha polisi.

Unaweza kuwaomba polisi wawasiliane na mtu mwingine ili kumjulisha kuwa uko katika kituo cha polisi. Anaweza kuwa mwanafamilia, mwenzi, mlezi wako, rafiki yako au mtu mwingine unayemjua. Watawasiliana na mtu huyo haraka iwezekanavyo.

### Ikiwa una umri wa chini ya miaka 16 (au hujafikisha miaka 18 na uko chini ya uangalizi)

- Polisi lazima wajaribu kumjulisha mzazi au mlezi wako kuwa uko kituoni.
- Mzazi au mlezi wako anaweza kuja na kukusaidia kituoni humo.

- Kupata usaidizi wa mkalimani

Ikiwa huzungumzi au huelewi lugha ya Kiingereza, polisi watamwalika mtu anayezungumza lugha yako (mkalimani) akusaidie. Hutalipishwa kwa hili. Ni muhimu kuelewa kinachosemwa katika kituo cha polisi.

Ikiwa wewe ni kiziwi au una matatizo ya kuwasiliana, polisi watamleta mtu wa kukusaidia. Huyu anaweza kuwa mkalimani wa Lugha ya Ishara ya Kiingereza au mtaalamu mwingine anayefaa. Hutalipishwa kwa hili.

- Ikiwa wewe si Mwingereza

Ikiwa wewe si Mwingereza, unaweza kuwaomba polisi wawasiliane na Ubalozi wako, ili kuwajulisha ulipo na kwa nini umezuiliwa katika kituo cha polisi. Wanaweza pia kukutembelea faraghani na kupanga wakili akuone.

- Je, nini kitatokea ukishtakiwa?

Ukishtakiwa kwa kosa, unaweza kuachiliwa kutoka kizuizini au unaweza kusalia katika kituo cha polisi na kupelekwa mahakamani siku inayofuata ya kazi. Au unaweza kuachiliwa ukikubali kwenda mahakamani tarehe iliyowekwa.

- Kupewa stakabadhi

Kesi yako ikipelekwa mahakamani, wewe au wakili wako atapewa taarifa ya ushahidi. Hii itakuwezeshau wewe au wakili wako kuandaa utetezi wako.

Una haki ya kupata huduma ya utafsiri wa taarifa husika ikiwa huelewi lugha ya Kiingereza.

- Kupata usaidizi wa kimatibabu

Polisi watakuuliza maswali kuhusu afya na hali yako. Ni muhimu uwajulishe polisi ikiwa una tatizo la kiafya au unatumia dawa. Pia ni muhimu uwajulishe polisi ikiwa una uraibu wowote wa dawa za kulevya au pombe au ikiwa unafikiria kujidhuru.

Polisi wanaweza kumwomba daktari akuchunguze. Hii huhakikisha unatunzwa ipasavyo ukiwa chini ya uangalizi. Wajulishe polisi ikiwa unahitaji kumwona daktari.

Ukiugua, una haki ya kupata usaidizi wa kimatibabu.

- Chakula na Vinywaji

Ukihitaji utapewa maji. Utapewa chakula ikiwa uko chini ya uangalizi kwa muda wa zaidi ya saa nne. Ikiwa una mahitaji yoyote ya chakula au kidini basi wajulishe polisi mapema iwezekanavyo.

- Kuwasilisha malalamiko

Ikiwa unataka kuwasilisha malalamiko ukiwa chini ya uangalizi, zungumza na Inspekta au afisa wa cheo cha juu. Ikiwa unataka kuwasilisha malalamiko baada ya kuachiliwa, unaweza kwenda kituo chochote cha polisi au upige simu kwa 101. Unaweza pia kumwomba mtu mwingine awasilishe malalamiko kwa niaba yako, mradi tu umetoa idhini hiyo kwa kuiandika. Inaweza kuwa mzazi, rafiki, mwenzi au mtu unayemwamini.

Ikiwa umeumizwa au kujeruhiwa na afisa wa polisi wakati wa kukamatwa au ukiwa chini ya uangalizi wa polisi unapaswa kuwasilisha malalamiko kwa Idara ya Viwango vya Kitaalamu Inayosimamia Polisi Nchini Uskoti (Police Scotland Professional Standards Department).

### Ikiwa unahitaji usaidizi wa ziada (tafadhali kumbuka, hii ni taarifa kuhusu huduma pekee na sio haki):

Huenda ukahitaji usaidizi kuelewa kinachotendeka ukiwa katika kituo cha polisi. Unaweza kupewa usaidizi huu kupitia msaidizi anayejulikana kama Mtu Mzima Husika. Unaweza kutumia huduma hii ikiwa una matatizo ya kiakili au ulemavu wa kujifunza. Zungumza na polisi ikiwa unahitaji usaidizi huu.

Ikiwa polisi wanaamini kwamba unahitaji usaidizi wa Mtu Mzima Husika, watamwalika aje, hata ikiwa hujaomba hilo.

## 2. Taarifa kwa watakaohojiwa na polisi

### • Kupata wakili wa kukusaidia

Waambie polisi ikiwa unataka kuzungumza na wakili. Polisi watawasiliana na wakili kwa ajili yako haraka iwezekanavyo.

Jukumu la wakili ni kulinda haki zako na kukupa ushauri kuhusu sheria.

Unaweza kuchagua kuzungumza na wakili unayemjua au wakili wa zamu anayepatikana. Wakili huyu ni huru na hafanyi kazi na polisi.

Wakili atakujulisha ikiwa atakushauri bila kukulipisha au ikiwa utalazimika kulipia ushauri. Iwapo unahitaji kumlipa, atakueleza kiasi na jinsi unavyoweza kulipia. Polisi hawatamlipa wakili wako au kujadili jinsi utakavyomlipa wakili wako.

Unaruhusiwa kufanya mazungumzo ya faragha na wakili kabla ya polisi kukuhoji isipokuwa iwe polisi wanahitaji kukuuliza maswali yanayoambatana na kuwepo kwa dharura, kwa sababu za kiusalama.

Unaweza kubadilisha uamuzi wako wa kuzungumza na wakili wakati wowote. Waambie polisi haraka iwezekanavyo na watawasiliana na wakili kwa ajili yako.

Wakili asipofika katika kituo cha polisi baada ya kuahidi kuwa atafika, au ikiwa unahitaji kuzungumza na wakili tena, waombe polisi wawasiliane naye tena.

Una haki ya kuwa na wakili chumbani polisi wanapokuhoji isipokuwa unahitaji kuuliwa maswali ya dharura kabla ya wakili kufika, kwa sababu za kiusalama.

### • Je, unaweza kuzuiliwa kwa muda gani ili kuhojiwa?

Polisi wanaweza kukuzuilia ili kukuhoji kwa hadi saa 48 bila kukushtaki kwa kosa lolote. Hata hivyo, afisi mkuu wa polisi anahitajika kuchunguza kisa chako ili kuona ikiwa bado unapaswa kuzuiliwa. Huu unajulikana kama ukaguzi. Unaweza tu kuzuiliwa kwa zaidi ya saa 48 ikiruhusiwa na mahakama. Mahakama inaweza kuongeza muda wa kuzuiliwa bila kufunguliwa mashtaka hadi siku zisizozidi 14 tangu kukamatwa kwako. Katika hali hizi, lazima upewe yafuatayo:

- Hati iliyoandikwa kwamba ombi la kuongeza muda wako wa kuzuiliwa limewasilishwa;
- Wakati ombi liliwasilishwa;
- Wakati ambapo ombi hili litasikilizwa mahakamani; na
- Sababu za kuzuiliwa zaidi.

Sharti upewe notisi (pamoja na mwakilishi wako wa kisheria) kila wakati ombi linapowasilishwa la kuongeza muda wako wa kuzuiliwa.

Wewe na wakili wako mna haki ya kutoa maoni yenu kuhusu uamuzi huu, isipokuwa iwe hali yako haikuruhusu kufanya hivyo. Wakili anaweza kukushauri kuhusu hili.

- Wageni Huru wa Uangalizi

Wapo wanajamii wanaoruhusiwa kuingia kwenye vituo vya polisi. Wanajulikana kama Wageni Huru wa Uangalizi na hufanya kazi kwa hiari ili kuhakikisha kuwa watu waliozuiliwa wanatendewa ipasavyo na wanapata haki zao.

Huna haki ya kumwona Mgeni Huru wa Uangalizi au kumwomba akutembelee lakini mgeni anaweza kuomba kukuona. Mgeni Huru wa Uangalizi akikutembelea ukiwa kizuizini atafanya hivyo bila kutegemea polisi ili kuhakikisha kwamba maslahi na haki zako zimelindwa. Kuzungumza naye ni kwa hiari.